# TAPAHR

## JUMUIYA YA MAAFISA TAWALA NA RASILIMALIWATU TANZANIA.

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

Aprili,2023

## Table of Contents


UTANGULIZI ........ 3

SEHEMU YA KWANZA ........ 4

TAFSIRI, JINA NA ANUANI ........ 4

SEHEMU YA PILI ........ 5

DIRA, DHIMA, NA MADHUMUNI YA JUMUIYA ........ 5

SEHEMU YA TATU ........ 6

IBARA YA 8: Aina ya Uanachama ........ 6

SEHEMU YA NNE ........ 8

UONGOZI, SIFA NA MAJUKUMU ........ 8

IBARA YA 13: Uiongozi wa Jumuiya ........ 8

IBARA YA 14: Sifa za Viongozi wa Jumuiya ........ 8

SEHEMU YA NNE ........ 10

VYOMBO VYA UTAWALA NA MAJUKUMU ........ 10

IBARA YA 18: VYOMBO VYA UTAWALA ........ 10

IBARA YA 19: MAJUKUMU YA VYOMBO VYA UTAWALA ........ 11

SEHEMU YA TANO ........ 12

MIKUTANO ........ 12

IBARA YA 20: AINA YA MIKUTANO ........ 12

**SEHEMU YA SITA** ........ 14

**MENGINEYO** ........ 14

IBARA YA 23: USHIRIKIANO ........ 14



REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

UTANGULIZI

**Kwa kutambua** umuhimu wa Taaluma ya Rasilimaliwatu na Utawala katika Utumishi wa Umma, ikiwa ndio taaluma inayosimamia rasimaliwatu kwa lengo la kuwezesha kusimamia rasimali nyingine ziweze kuwa na tija kwa kutoa metokeo yaliyokusudiwa;

**Kwa kufahamu kwamba**, ili kuwa na wanataaluma wanaojituma, waadilifu wenye ujuzi, weledi na wenye hamasa ya kuleta tija na maendeleo katika Nchi; na

**Kwa kuzingatia kwamba,** lengo ni kujenga, kukuza na kuendeleza umoja na ushirikiano katika Taaluma ya Maafisa Rasilimaliwatu na Utawala, kujenga uhusiano na Jumuiya zingine zinazohusu taaluma ya Rasimaliwatu na Utawala pamoja na kuwa na jukwaa litakalo endeleza Taaluma hii inayobadilika kila wakati;

**Sisi** Maafisa Rasilimaliwatu na Maafisa Utawala kwa pamoja tumeamua na kukubaliana kuanzisha Jumuiya hii itakayojulikana kwa ina la "**Jumuiya ya Maafisa Tawala na Rasilimaliwatu Tanzania"** na kutengeneza Katiba hii ili iwe Mwongozo katika utekelezaji wa shughuli zote za Jumuiya.

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

SEHEMU YA KWANZA

TAFSIRI, JINA NA ANUANI

IBARA YA 1: Tafsiri,

Katika Katiba hii maneno yafuatayo yatakuwa na tafsiri kama ilivyoainishwa chini ya Ibara hii na si vinginevyo: -

a. "**Afisa Rasilimaliwatu**" ni mtumishi wa umma mwenye sifa stahiki kama zilivyoainishwa kwenye Muundo wa Maendeleo ya Utumishi wa Maafisa Utumishi;

b. "**Afisa Tawala**" ni mtumishi wa umma mwenye sifa stahiki kama zilivyoainishwa kwenye Muundo wa Maendeleo ya Utumishi wa Maafisa Tawala;

c. **"Bodi ya Wadhamini"** ni chombo ndani ya Jumuiya kitakacho simamamia mali za Jumuiya zinazohamishika na zisizohamishika kwa niaba ya Wanachama;

d. **"Jumuiya**" inamaanisha Jumuiya ya Maafisa Tawala na Rasilimaliwatu Tanzania;

e. **"TAPAHR" ina** maana ya Jumuiya ya Maafisa Tawala na Rasilimaliwatu Tanzania;

f. **"Katiba"** kwa muktadha huu itamaanisha Katiba ya Jumuiya ya Maafisa Tawala na Rasilimaliwatu Tanzania;

g. "**Mwanachama**" kwa tafsiri ya Katiba hii Mtumishi wa Umma au Taasisi iliyokidhi masharti ya katiba na kujisajiri katika chama.

h. **"Mwanachama hai"** ni mwanachama ambaye amechangia michango yake yote ya uanachama kwa mujibu wa Katiba hii.

i. **"Mtumishi wa Umma"** ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298.

IBARA YA 2: Jina la Jumuiya

2.1 Jumuiya hii inajulikana kama "Jumuiya ya Maafisa Tawala na Rasilimaliwatu Tanzania." (TAPAHR)

2.2 Katiba hii itarejewa na kujulikana kama Katiba ya Jumuiya ya Maafisa Tawala na Rasilimaliwatu Tanzania, 2023.

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

IBARA YA 3: Anuani ya Jumuiya

3.1 Isipokuwa pale ambapo kutatokea mabadiliko yoyote yatakayoidhinishwa kwa mujibu wa Katiba hii, anuani ya Jumuiya itakuwa :-

Mwenyekiti,
Jumuiya ya Maafisa Tawala na Rasilimaliwatu Tanzania" (TAPAHR),
S.L.P. 670,
**DODOMA**

Barua pepe;
Tovuti;

3.2 Ofisi ya Jumuiya itakuwa katika Ofisi/Wizara inayoshughulikia Utumishi wa Umma, au eneo jingine lolote ambalo wanachama wataridhia.

3.3 **Hadhi ya Jumuiya**

Jumuiya ya Maafisa Tawala na Rasilimaliwatu Tanzania, imeanzishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Jumuiya, Sura 337.

IBARA YA 4: Lugha

Katika utendaji wa shughuli zake, Jumuiya itatumia lugha ya Kiswahili katika vikao vyake vyote na lugha ya Kiswahili au Kiingereza kwa mawasiliano ya kimaandishi.

SEHEMU YA PILI

DIRA, DHIMA, NA MADHUMUNI YA JUMUIYA

**IBARA YA 5: Dira**

Kuhakisha ufanisi na uweledi kwa Maafisa Rasilimaliwatu na Maafisa Tawala katika Utumishi wa umma ili kuleta tija iliyokusudiwa kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**IBARA YA 6: Dhima**

Kukuza viwango na mifumo bora ya taaluma ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Utawala katika Utumishi wa Umma.

**IBARA YA 7: Malengo ya Jumuiya**

7.1 Kuanzisha jukwaa la kitaifa la Maafisa Rasilimaliwatu na Maafisa Tawala katika Utumishi wa Umma ili kupata fursa ya kubadilishana uzoefu katika masuala ya usimamizi wa Rasilimaliwatu na utawala.

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

7.2 Kukuza ujuzi na weledi katika eneo la usimamizi wa Rasilimaliwatu na Utawala wa Umma miongoni mwa wanachama na wasimamizi wengine,

7.3 Kuhifadhi na kusambaza taarifa za kitaaluma katika Kada ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Utawala kwa njia ya tafiti, machapisho, mikutano, ziara za mafunzo, makongamano ya kitaalamu, midahalo na kuweza kujiunga na mitandao ya kitaaluma (professional networks) kitaifa na kimataifa,

7.4 Kuimarisha maadili ya kitaaluma kwenye masuala yanayohusu Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Utawala,

7.5 Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa kupitia mashirika na taasisi zinazojishughulisha na ukuaji wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Utawala

7.6 Kuimarisha utekelezaji wa mifumo yenye matokeo tarajiwa na shirikishi ya kiutawala ili kufanikisha huduma bora kwa Umma.

## SEHEMU YA TATU
## UANACHAMA

IBARA YA 8: Aina ya Uanachama

8.1 **Uanachama wa uanzilishi**
Ni mwanachama aliyesaidia katika mchakato mzima wa kuanzisha Jumuiya hii.

8.2 **Uanachama wa Kawaida**
Ni mwanachama anayejiunga kwa kuwasilisha maombi maalum.

8.3 **Uanachama wa Heshima**
Atakuwa mtu yeyote, Kampuni au Taasisi itakayependekezwa na Kamati Tendaji na kuchaguliwa katika Mkutano Mkuu wa mwaka kwa kuzingatia;
i) Mchango aliochangia/iliyochangia katika kuendeleza taaluma ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Utawala.
ii) Mchango anaotoa kwa ajili ya kufadhili na kukuza Jumuiya.

**IBARA YA 9: Sifa ya Mwanachama**

9.1 Mtu yeyote ambaye anahitaji kujiunga na Jumuiya atatakiwa kutimiza masharti yafuatayo;



REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

i. Awe anahusika au amekuwa akijishughulisha kikamilifu katika Taaluma ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Utawala
ii. Mwenye sifa za kitaaluma za Rasilimali na Utawala.
iii. Awe mtumishi wa Umma, na
iv. Awe tayari kuzingatia Katiba

9.2 Bila kuathiri Ibara ya 9.1 masharti yaliyoainishwa katika kipengele cha (iii) hayatatumika kwa wanachama wa heshima.

**IBARA YA 10: Ada za Uanachama**

10.1 Ada ya kujiunga uanachama ni Shillingi Elfu hamsini ( 50,000/=) na Ada ya kila mwaka ni Shillingi laki mbili (200,000/=).

10.2 Ada ya uanachama wa Heshma ni Shillingi laki tano (500,000/=) na Ada ya mwaka ni Shillingi Millioni Moja (1,000,000/=)

10.3 Ada ya uanachama na Ada ya kila mwaka zinaweza kubadilika mara kwa mara na mabadiliko hayo yataidhinishwa na Mkutano Mkuu.

10.4 Malipo yote ya Ada yatafanyika kupitia akaunti ya Jumuiya na Mhazini atahakikisha anatoa stakabadhi ya kila malipo yaliyolipwa.

**IBARA YA 11: Haki na Wajibu wa Mwanachama**

11.1 Kulingana na masharti yaliyowekwa na Katiba hii, kila mwanachama atakuwa na haki zifuatazo:-

a) Kushiriki na kuchangia katika Mkutano Mkuu wa Jumuiya;
b) Haki ya kupiga kura;
c) Haki ya kujitetea na kupewa nafasi ya kusikilizwa pale anapoitwa na Kamati yoyote kujieleza kuhusu tuhuma zozote zinazomkabili;
d) Kushiriki na kutoa maamuzi katika shughuli zote za Jumuiya;
e) Kuchagua ama kuchaguliwa kushika nafasi yoyote ya uongozi kulingana na masharti yatakayowekwa;

11.2 Kila mwanachama atakuwa na wajibu kama ifuatavyo:-

a) Kulipa ada ya kila mwaka kwa wakati.
b) Kuhudhuria mikutano yote halali ya Jumuiya na kuheshimu uendeshaji wa mkutano husika;
c) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za Jumuiya kama itakavyo amuliwa na kukubaliwa na wanachama;
d) Kufahamu na kusimamia Katiba na kanuni mbalimbali za Jumuiya;
e) Kutofanya jambo lolote lisilo na maslahi kwa Jumuiya na likalochafua taswira ya Jumuiya au Wanachama mbele ya jamii.

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

**IBARA YA 12: Ukomo wa Uanachama**

12.1 Mwanachama atapoteza sifa za uanachama endapo, mojawapo au zaidi ya haya yafuatayo litatokea:-

a) Iwapo atafariki
b) Iwapo Utumishi wake wa umma utakoma kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298
c) Endapo ataacha uanachama kwa hiari yake,
d) Endapo atafukuzwa uanachama na Mkutano Mkuu;

SEHEMU YA NNE

UONGOZI, SIFA NA MAJUKUMU

IBARA YA 13: Uiongozi wa Jumuiya

13.1 Jumuiya itaundwa na Viongozi Wakuu wafuatao;

a) Mwenyekiti
b) Makamu wa Mwenyekiti
c) Katibu
d) Mhazini

IBARA YA 14: Sifa za Viongozi wa Jumuiya

14.1 Viongozi wa Jumuiya wanapaswa kuwa na Sifa zifuatazo:-

a) Mwanachama hai wa Jumuiya
b) Mwenye Taaluma ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu au Utawala
c) Awe ametumikia Utumishi wa Umma kuanzia ngazi ya Afisa Mwandamizi
d) Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai au kuchukuliwa hatua zozote za kinidhamu katika Utumishi wa Umma zilizopelekea kupewa adhabu.
e) Awe anaijua Katiba na kuweza kuitetea.

**IBARA YA 15: Majukumu ya Viongozi**

**15.1 Mwenyekiti**

a) Msimamizi Mkuu wa masuala yote ya Jumuiya
b) Atakuwa ndiye Msemaji wa masuala yote yanayohusu Jumuiya
c) Ataongoza vikao vyote vya Kamati Tendaji, Mkutano Mkuu na Mkutano Mkuu Maalum wa Jumuiya
d) Atakuwa ndiye mtia saini kwenye nyaraka zote rasmi za Jumuiya
e) Mdhibiti Mkuu wa Fedha na mali za Jumuiya

**15.2 Makamu Mwenyekiti**

a) Msaidizi Mkuu wa Mwenyekiti
b) Atatekeleza majukumu ya Mwenyekiti pale ambapo Mwenyekiti hayupo



REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

c) Kutekeleza majukumu yoyote atakayoelekezwa na Mwenyekiti.

**15.3 Katibu**

a) Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu na kiungo kati ya vyombo mbalimbali vya Jumuiya
b) Mtekelezaji Mkuu wa maamuzi ya Jumuiya.
c) Atakuwa ni Katibu wa vikao na mikutano ya Jumuiya
d) Mratibu wa shughuli zote zilizoamuliwa kutekelezwa na vikao na mikutano ya Jumuiya
e) Ataanda na kuratibu mikutano, vikao vya Jumuiya kama vile semina, tafiti, na safari za kujifunza (study tour)
f) Atasimamia utendaji kazi wa jumla wa Jumuiya
g) Ataandaa Taarifa za Utekelezaji wa masuala mbalimbali katika Jumuiya yaliyoagizwa na Vikao / Mkutano Mkuu na kuwasilisha mrejesho kwenye vikao.
h) Ataratibu uhifadhi wa Taarifa na Takwimu mbalimbali za Jumuiya kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya Jumuiya
i) Atahuisha kanzidata ya wanajumuiya kwa muda wote.

**15.4 Mhazini**

a) Msimamizi /Mhifadhi wa Rasilimali Fedha za Jumuiya ;
b) Kutunza kumbukumbu za kudumu za fedha na miamala mbalimbali ya fedha inayofanywa na Jumuiya;
c) Atasimamia maandalizi ya Bajeti ya kila mwaka ya Jumuiya na kuwasilisha katika vikao husika kuidhinishwa;
d) Kufanya malipo kama ankara za madai na Manunuzi mbalimbali kwa watoa huduma ambayo yameidhinishwa na Jumuiya kupitia vikao vyake;
e) Kusimamia na kuratibu makusanyo ya ndani ya Jumuiya (kiingilio, ada ya mwaka na ufadhili mbalimbali);
f) Kuandaa Taarifa ya Mapato na Matumizi ya kila robo mwaka na Mwaka na kuwasilisha katika vikao husika;
g) Atakuwa Mshauri Mkuu wa masuala ya kifedha kwa Kamati Tendaji;
h) Kufunga Hesabu za Jumuiya za kila mwaka na kuwasilisha Taarifa iliyokaguliwa kwenye Mkutano Mkuu.

**IBARA YA 16: Uchaguzi wa Viongozi**

16.1 Viongozi wote watachaguliwa na wanachama wa Jumuiya katika Mkutano Mkuu wa Jumuiya.
16.2 Mkutano Mkuu utakuwa halali endapo theluthi mbili ya wanachama watahudhuria.

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2918
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

16.3 Uchaguzi utafanyika kwa njia ya kupiga kura ya siri kwa kutumia karatasi maalum zitakazoandaliwa na kamati ya uchaguzi

16.4 Atakaye pata kura nyingi zaidi ya mwenzake ndiyo atakae kuwa Kiongozi

16.5 Endapo kura zilizopigwa zimefungana mchakato wa kupiga kura utaanza upya.

**IBARA YA 17: Ukomo wa Viongozi**

17.1 Kiongozi atastahili kukaa katika uongozi kwa muda wa miaka 3 na atakuwa na sifa ya kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

17.2 Uanachama wake utakapositishwa kwa mujibu wa Ibara ya 12 ya Katiba hii.

17.3 Kukoma uongozi kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake

SEHEMU YA NNE

VYOMBO VYA UTAWALA NA MAJUKUMU

IBARA YA 18: VYOMBO VYA UTAWALA

**18.1 Kamati Tendaji**

Kutakuwa na Kamati Tendaji itakayoundwa na Viongozi Wakuu wa Jumuiya na wajumbe watano ambao watachaguliwa katika Mkutano Mkuu wa Jumuiya. Vikao vya Kamati Tendaji vitafanyika mara nne kwa mwaka kabla ya Mkutano Mkuu kufanyika. Kikao hicho **kitakuwa halali** kukaa iwapo akidi yake itafika zaidi ya nusu ya wajumbe wote wa Kamati Tendaji.

**18.2 Kamati ya fedha**

Kutakuwa na Kamati ya fedha itakayoundwa na wajumbe wafuatao;

(i) Mweka Hazina wa Jumuiya ambaye atakuwa Mwenyekiti

(ii) Afisa wa Jumuiya aliyeajiriwa mwenye taaluma na masuala ya uhasibu,

(iii) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Mwenyekiti wa Jumuiya kutoka miongoni mwa Viongozi wakuu wa Jumuiya,

(iv) Mjumbe mmoja atakayechaguliwa na Mkutano Mkuu wa Jumuiya.

**18.3 Sekretarieti**

Mwenyekiti atakuwa na Mamlaka ya kuteua wanachama watano (5) watakaounda Sekretarieti ambao wataidhinishwa na Kamati Tendaji.

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

### 18.4 Bodi ya Wadhamini

Kutakuwa na Bodi ya Wadhamini itakayoundwa na watu watano watakaochaguliwa kwenye Mkutano Mkuu.

18.4.1 Bodi hii itaundwa na watu waliojitolea kukisaidia Chama kwa hali na mali, katika kuhakikisha malengo ya Chama yanafikiwa kwa kujitolea kwao kwa fedha, ushauri na mali

18.4.2 Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini utafanywa na Mkutano Mkuu wa Jumuiya kufuatia mapendekezo yatakayokuwa yametolewa na Kamati Tendaji

18.4.3 Ili kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi la Waadhamini mhusika atatakiwa kuwa hana nafasi yoyote ya uongozi ndani ya Jumuiya

18.4.4 Mdhamini atastahili kukaa katika nafasi yake kwa muda wa miaka 3 na atakuwa na sifa ya kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

18.4.5 Ili kuwa na sifa ya kuchaguliwa kuwa katika Bodi ya Wadhamini mwanachama awe na cheo cha Afisa Mwandamizi

18.4.6 Ukomo wa Mdhamini wa Jumuiya utakoma iwapo;

i. Atafariki
ii. Kwa hiari yake, atakapoacha uanachama;
iii. Mkutano Mkuu wa Jumuiya kupitia pendekezo litakalokuwa limetolewa na Kamati Tandaji, utaazimia kuwa mjumbue amekosa sifa za kuendelea kuwa mjumbe wa Bodi ya Wadhamini.

IBARA YA 19: MAJUKUMU YA VYOMBO VYA UTAWALA

19.1 Majukumu ya Kamati Tendaji

a) Kusimamia shughuli za kila siku za jumuiya
b) Kutoa taarifa ya mwaka ya shughuli za Jumuiya kwenye Mkutano Mkuu wa mwaka.
c) Kuendeleza na kusimamia shughuli mbalimbali za maendeleo za Jumuiya.
d) Kupokea maombi ya wanachama wapya.
e) Kujadili na kupendekeza adhabu kwa mwanachama aliyekiuka taratibu na Kanuni za Jumuiya.
f) Kupendekeza majina ya Bodi ya Wadhamini.

19.2 Majukumu ya Kamati ya Fedha

a) Kupokea rasimu ya Bajeti, kuijadili na kuiboresha rasimu hiyo kabla haijawasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Jumuiya.

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

b) Kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala yanayohusu utunzaji wa rasilimali na fedha za Jumuiya.
c) Kupokea, kujadili na kuandaa taarifa ya hoja za Mkaguzi wa nje wa Hesabu za Fedha za Jumuiya ikiwepo taarifa ya Mkaguzi wa Ndani na Kuwasilisha taarifa na mapendekezo mbele ya Kamati Tendaji.

19.3 Majukumu ya Sekretarieti
a) Kutekeleza majukumu ya kiofisi kama itakavyoelekezwa na Katibu
b) Kufanya maandalizi ya vikao na mikutano
c) Kuandaa mihutasari ya vikao na mikutano kwa usahihi
d) Kuratibu mahudhurio ya wajumbe katika vikao na mikutano
e) Kusaidia maandalizi ya Taarifa mbalimbali za Jumuiya kama itakavyokuwa imeelekezwa na Katibu
f) Kuwa kiungo kati ya wajumbe/wanachama na Uongozi wa Jumuiya kwa muda wote wa vikao, mikutano hata pasipo kuwa na mikutano au vikao.
g) Ni chombo kikuu cha utekelezaji na kitawajibika kwa Katibu

19.4 Majukumu ya Bodi ya Wadhamini
a) Kusimamia mali zote za Jumuiya
b) Kushauri vyombo vya utawala wa Jumuiya uendeshaji bora wa shughuli za chama.
c) Kutoa ushauri utakao saidia kukuza Taaluma ya Maafisa Utumishi na Maafisa Utawala.
d) Kutekeleza majukumu mengine yoyote ambayo yatakabidhiwa kwake na Mkutano Mkuu.

SEHEMU YA TANO
MIKUTANO

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

IBARA YA 20: AINA YA MIKUTANO

**20.1 Mkutano Mkuu**

Mkutano Mkuu wa Jumuiya utafanyika mara moja kwa mwaka na Mkutano huu utakuwa ndio mkutano utakaotoa maamuzi ya mwisho katika usimamizi wa shughuli zote za Jumuiya wa ngazi ya juu,

a) Taarifa ya Mkutano Mkuu itatolewa kwa wajumbe ndani ya siku 30 kabla ya mkutano huo,

b) Akidi ya Mkutano Mkuu isipungue theluthi mbili ya wanajumuiya wote. Akidi hii isipotimia Mkutano huo utaahirishwa na kupangwa siku nyingine. Hata hivyo kwa mkutano unaofuata iwapo hautakidhi akidi kwa mara nyingine, Mkutano huo utachukuliwa kuwa ni mkutano halali,
c) Mkutano Mkuu utakuwa na jukumu la kuchaguwa viongozi wapya iwapo muda wa viongozi/kiongozi aliyepo umefika ukomo,
d) Utakuwa na jukumu la kupitia na kujadili taarifa za jumuiya za mwaka ikiwemo kuthibitisha, kurekebisha au kutothibitisha taarifa za Kamati Tendaji,
e) Kupokea na kujadili hesabu za mwaka, muhtasari wa Taarifa za ukaguzi wa fedha,
f) Kupokea makisio ya Bajeti ya Jumuiya kwa mwaka unaofuata,
g) Kujadili marekebisho ya Katiba iwapo itaonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

**20.2 Mkutano wa Dharura**

Mkutano wa dharura utaitishwa katika mazingira yafuatayo: -

(a) Wanachama watawasilisha kwa Mwenyekiti maombi ambayo yataainisha sababu za msingi kuomba kuitisha mkutano huo. Maombi hayo yataambatana na muhtasari ambao utakuwa umesainiwa na wanachama hao. Baada ya maombi hayo kuwasisilishwa na kukubaliwa, Mwenyekiti atamtaarifu Katibu kwa ajili ya kupanga siku ya kuitisha Mkutano huo.
(b) Akidi ya Mkutano wa dharura inatakiwa kuwa na wanachama wasiopungua theluthi mbili ya wanachama wote.
(c) Endapo Mwenyekiti atashindwa kuitisha Mkutano wa dharurua ndani ya miezi mitatu baada ya kupokea taarifa ya maombi, wanachama watakua na haki ya kuitisha Mkutano Mkuu wa dharura.

IBARA YA 21 MASUALA YA KIFEDHA NA WAWEKA SAINI

21.1 Katika masuala yoyote ya kifedha hususan kutoa fedha zilizopo kwenye akaunti ya Jumuiya, nyaraka na mikataba ambayo Jumuiya itaingia, makundi yafuatayo yatakuwa na sifa ya kusaini nyaraka hizo;

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

**Kundi A;**
1. Mwenyekiti
2. Mhazini
3. Mjumbe mmoja kutoka kwenye Kamati ya Utendaji

**Kundi B**;
1. Makamu Mwenyekiti
2. Katibu
3. Mjumbe mmoja kutoka kwenye Kamati Tendaji

21.2 Wajumbe wawili watasaini kwa wakati mmoja ikiwa mmoja kutoka kundi A na mmoja kutoka Kundi B

21.3 Nyaraka zote za kiuhasibu zataandaliwa na Mkaguzi wa Hesabu wa ndani ambaye atakuwa Mwajiriwa wa Jumuiya.

IBARA YA 22 TARATIBU ZA AJIRA

22.1 Jumuiya itaajiri watumishi kwa ngazi mbalimbali ili kuweza kutekeleza majukumu mbalimbali ya kiutendaji endapo itaonekana inafaa kufanya hivyo.
22.2 Katibu atahusika na utaratibu wa kuajiri watumishi kwa masharti ya mkataba kufuatia ridhaa ya Kamati Tendaji.
22.3 Taratibu za ajira katika Jumuiya zitakuwa kwa ushindani na atakayepata alama za juu ndiye atakayeajiriwa.

**SEHEMU YA SITA**
**MENGINEYO**

IBARA YA 23: USHIRIKIANO

23.1 Jumuiya inaweza kushirikiana na Jumuiya zingine za Kitaifa, Kikanda, na Kimataifa ilimradi ushirika huo unaendana na malengo ya Jumuiya na kwa kiwango kinachoruhusiwa na Katiba hii.
23.2 Jumuiya ya AAPAM -Tanzania Chapter na Jumuiya ya APS-HRMNET kama Taasisi zinazojitegemea zitakuwa zinatambuliwa katika Jumuiya hii.

IBARA YA 24: MAREKEBISHO YA KATIBA

24.1 Endapo kutatokea uhitaji wa marekebisho ya Katiba hii, wanachama watatoa mapendekezo ya maandishi ambayo yatabainisha kipengele ambacho kinakusudiwa kufanyiwa

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

marekebisho. Mapendekezo hayo yatawasilishwa kwenye Kamati Tendaji.

24.2 Kamati Tendaji itajadili mapendekezo hayo na kuyawasilisha katika Mkutano Mkuu wa Jumuiya ambapo utatolewa uamuzi wa mwisho.

24.3 Katiba inaweza kubadilishwa na Mkutano Mkuu baada ya robo tatu (3/4) ya Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu kukubali mabadiliko husika.

24.4 Mkutano Mkuu utakuwa ndiyo chombo pekee chenye mamlaka ya kupitisha mabadiliko yoyote ya Katiba hii au kupitisha azimio la uundwaji wa Katiba Mpya.

**IBARA YA 25 KUTUNGA KANUNI**

Jumuiya itaanda kanuni ambazo zitaainisha masuala mbalimbali kwa ajili ya urahisi wa utekelezaji wa Katiba hii.

**IBARA YA 26 KIPINDI CHA MPITO**

Viongozi wote wa Jumuiya waliopo wakati wa kupitishwa Katiba hii wataendelea na nafasi zao kwa kipindi cha miaka miwili toka tarehe ambayo Msajili ataidhinisha Katiba hii na baada ya hapo utaratibu wa kuchagua viongozi kwa kuzingatia Katiba utafuatwa.

IBARA YA 27: KUVUNJWA KWA JUMUIYA

Jumuiya inaweza kuvunjwa kutokana na sababu zifuatazo; -

27.1 Endapo wanachama watapungua kufikia wanachama 20.

27.2 Endapo kutakua na maombi ya msingi ya wanachama yasiopungua robo tatu (¾) ya wanachama wote wakiomba jumuiya hiyo ivunjwe.

27.3 Kutokana na amri ya Msajili, amri ya Mahakam au amri ya Rais wa Jamhuri ya Muungani wa Tanzania.

27.4 Endapo Jumuiya itavunjwa mambo yafuatayo yatazingatiwa;-

a) Mali zote zinazohamishika na zisizohamishika baada ya amri ya kuvunjika kwa Jumuiya kutolewa, zitawekwa chini ya Bodi ya Wadhamini,
b) Malipo ya madeni yote ya Jumuiya kama yatakuwepo,
c) Uuzwaji wa mali za kudumu za Jumuiya,
d) Fedha zilizopo za Jumuiya baada ya kulipa madeni yote zitagaiwa kwa wanachama wote kwa kuzingatia michango yao.

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

IBARA YA 28: MUHURI WA JUMUIYA

Kutakuwa na muhuri wa Jumuiya ambao utatumika kwenye nyaraka zote zitakazo husiana na Jumuiya. Mwenye dhamana ya kuhifadhi muhuri huo ni Katibu.

IBARA YA 29: KUIDHINISHA NA MUDA WA KUANZA KUTUMIKA

Katiba hii imeidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Jumuiya uliofanyika tarehe .................

| Mwenyekiti | Katibu |
|---|---|
| Saini .............................. | Saini................................. |
| Jina ...................................... | Jina ................................... |
| Tarehe ................................. | Tarehe .............................. |

BARA YA 30

Katiba hii imeanza kutumika rasmi kuanzia tarehe .......................baada ya kupitishwa na Msajili wa Vyama vya kijamii.

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

IBARA YA 28: MUHURI WA JUMUIYA

Kutakuwa na muhuri wa Jumuiya ambao utatumika kwenye nyaraka zote zitakazo husiana na Jumuiya. Mwenye dhamana ya kuhifadhi muhuri huo ni Katibu.

IBARA YA 29: KUIDHINISHA NA MUDA WA KUANZA KUTUMIKA

Katiba hii imeidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Jumuiya uliofanyika tarehe 23/02/2023

Mwenyekiti

Saini Mavika

Jina LEKA MAVIKA

Tarehe 23/02/2023

Katibu

Saini Dmora

Jina DEBORA MWANGWAJI

Tarehe 23-02-2023

BARA YA 30

Katiba hii imeanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 23/02/2023 baada ya kupitishwa na Msajili wa Vyama vya kijamii.

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS